

Maswali na Majibu

1. Daudi alichukua mji gani kuwa mji wake mkuu? *Yerusalemu*
2. Kwa nini Daudi alitaka kuleta Sanduku la Mungu Yerusalemu?
Ili watu wote waje wakiabudu Mungu Yerusalemu.
3. Mungu alisema Sanduku lilitakiwa libebwe namna gani?
Makuhani walikuwa wabebe kwa miti mbili
4. Daudi alijaribu kuleta Sanduku Yerusalemu namna gani? Nini ilifanyika?
Juu ya gari la n'gombe. N'gombe alipojikwaa, Uza alishika Sanduku na akafa.
5. Daudi alifanya nini hasira ya Mungu iliporudi chini?
Alitumia makuhani kubeba na kulileta Yerusalemu na kwa furaha kubwa.
6. Mbona Daudi alitaka kujengea Mungu Hekalu?
Daudi alikuwa na nyumba ya kifahari hali Sanduku la Mungu lilikuwa kwa hema.
7. Mbona Mungu alisema kwamba Daudi hasitahili kumjengea Hekalu?
Kwa sababu alikuwa ni mtu aliyepigana vita vingi.
8. Ahadi zenye Mungu aliahidi kwa Daudi zinatufunza nini?
Kusudi ya Mungu kwa binadamu hapa duniani.
9. Nani alitimiza sehemu ya ahadi za Mungu? *Sulemani.*
10. Nani anatumiza hizo ahadi zote? *Yesu*

Mistari ya kukariri

1 Mambo ya Nyakati 17:11 – 12 Luka 1:30 – 33

Mazungumzo

Zungumza juu ya kila ahadi yenye Mungu aliambia Daudi na vile imetimizwa.

Kuandika

Andika vile Daudi alileta Sanduku Yerusalemu.

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 22 Daudi – mfalme mzuri

SOMA 2 Samweli 5:1 – 10; 6:1 – 15; 7:1 – 17

SOMO

Daudi alitawala kutoka mji wa Hebroni kwa miaka 7. Baadaye alichukuwa Yerusalemu pia na akaifanya kuwa mji wake mkuu. Wayebusi walikuwa wakiishi Yerusalemu. Mji wa Yerusalemu ulijengwa juu ya vilima. Kwa hivyo ilikuwa raisi Wayebusi kuikinga kutoka kwa Daudi, yaani hangeweza kuichukuwa. Wayebusi walisema Yerusalemu ni ya nguvu sana, hata viwete na vipofu wanaweza kuikinga.

Lakini Daudi aliichukuwa. Yoabu mwana jeshi mkuu wa Daudi alipanda juu ya mfereji wa maji. Watu wa Daudi waliwezesha kupanda juu mpaka kwa kuta za mji, hata wakashangaza Wayebusi. Daudi akaufanya mji wa Yerusalemu kuwa mji wake mkuu.

Yerusalemu ni mji uliochaguliwa na Mungu. Ulikuwa mji wa Waisraeli tena ni katikati penye waliabudia. Wakati mwingine Yerusalemu huitwa Sayuni; hili ni jina la moja ya vilima vyenye Yerusalemu imejengwa.

Daudi alitaka kuleta Sanduku la Mungu Yerusalemu ili watu waabudu Mungu kutoka kule. Sanduku la Mungu lilikuwa takatifu sana. Mungu alikuwa ameaambia Musa kwamba ni makuhani tu, ndio walitakiwa kubeba Sanduku; lazima wabebe kwa miti miwili. Mtu yeyote akiguzatakatifu.



Daudi alijaribu kuleta Sanduku Yerusalemu kwa gari la n'gombe. Walipofika penye wanapuria, n'gombe walijikwaa na Sanduku likatikisika. Mtu aitwaye Uza alijaribu kuzuia lisianguke, lakini alipoligusa, alikufa. Daudi aliogopa na akaliweka Sanduku kwa nyumba iliyokuwa karibu. Baadaye Daudi alipojua kwamba Mungu hana hasira, aliambia makuhani wabebe Sanduku na wapeleke Yerusalemu. Daudi pamoja na watu walifurahi na kutoa dhahibu. Sanduku la Mungu lililetwa Yerusalemu na watu walikuja kuabudu Mungu.

Daudi alipigana na mataifa mengi yaliyokuwa adui wa Israeli. Daudi aliamini Mungu kwa hivyo alishinda vita vyote na kuwa mfalme wa nguvu. Mungu alimpa Daudi amani kutoka kwa maadui wake.

Daudi alijenga jumba yake ya kifalme. Ilikuwa nyumba ya kifahari iliyojengwa kwa mierezi. Lakini Sanduku la Mungu lilikuwa bado linaishi kwa hema (Maskani). Daudi alitaka kujenga Hekalu yenye watu wangeabudia Mungu. Daudi aliambia nabii Nathani, "Mimi ninaishi kwa nyumba ya mierezi na Sanduku la Mungu liko ndani ya hema." Daudi alielezea Nathani kwamba alitaka kujengea Mungu Hekalu.

Mungu alimwambia Daudi kwamba hangemjengea Hekalu kwa sababu amekuwa mtu wa vita kwa muda mrefu. Ingawaje Mungu alifurahia Daudi kwa sababu alikuwa na nia ya Kumjengea Hekalu. Mungu alimbariki Daudi na kumwaahidi ahadi za kipekee. Hizi ahadi ni za maana sana. Zinatwambia zaidi juu ya sababu za Mungu na kwa watu.

Unakumbuka ahadi za Mungu kwa Ibrahimu? Mungu aliahidi Ibrahimu kwamba atakuwa na mzao mmoja wa kipekee mwenye kila mtu atabarikiwa kupitia kwake. Tena aliahidi kwamba wazao wa Ibrahimu watakaa katika nchi ya Israeli milele. Hizi ahadi zinatimizwa kwa Yesu Kristo. Kupitia kwa kifo Chake msalabani ameletea watu wote wokovu. Yesu atarudi hivi karibuni na watu wa Mungu wote watakuwa na amani na furaha katika Ufalme wa Mungu hapa duniani.

Katika ahadi za Mungu kwa Daudi, tunajifunza sana juu ya mipango ya Mungu kwa wanadamu na wokovu. Hizo ahadi ziko pale mbele.

Sulemani, mwanaye Daudi alikamilisha baadhi ya hizo ahadi. Lakini ahadi zingine zilielekezwa kwa mzao wa kipekee - Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Hivi karibuni Yesu akija hapa duniani atatimiza ahadi za Mungu zote. Yesu atasimamisha Ufalme wa Mungu na atatawala ulimwengu wote milele. Utakuwa wakati wa amani na furaha.

AHADI ZA MUNGU KWA DAUDI

Daudi atakuwa mtu wa ajabu, mmoja wa watu wakuu duniani

Daudi ni wa maana - bado tunasoma juu yake hata sasa, miaka 3000 nyuma! Alikuwa mmoja wa watu wakuu wa Mungu - alitwa mtu anayependeza moyo wa Mungu

Waisraeli watakuwa na nchi yao na wataishi kwa amani

Waisraeli walipata nchi yao. Walikuwa na amani wakati Daudi na Sulemani, mwanaye walitawala. Kutakuwa na amani kwa Ufalme wa Mungu.

Mungu ataimarisha nyumba ya Daudi

Nyumba ya Daudi (wazao) walitawala juu ya Yuda mpaka walipopelekwa mateka Babeli. Mwanawe alifwata baada ya baba yake mpaka waliposhikwa mteka. Tangu wakati huo, hakujakuwa na mzao wa Daudi kwa kiti chake cha enzi. Yesu ndiye mzaliwa wa kipekee wa Daudi. Atatawala kwa Ufalme wa Mungu.

Mzao wa Daudi atajengea Mungu Nyumba

Mungu aliambia Daudi kwamba hatajenga Hekalu. Sulemani, mwana wa Daudi ndiye alijenga Hekalu Yerusalemu. Hiyo Hekalu iliharibiwa wakati Waisraeli walichukuliwa mateka na Wakaldayo. Yesu ako anajenga Hekalu ya watu kuabudu Mungu kwa Ufalme Wake.

Mzao wa Daudi Atatawala MILELE kutoka kwa kiti cha enzi cha Daudi

Sulemani alitawala Waisraeli kutoka kwa kiti cha Daudi kwa miaka mingi na akafa. Yesu mzao wa Daudi wa kipekee, atatawala milele katika Ufalme wa Mungu hapa duniani. Yesu atatawala kutoka Yerusalemu kwenye kiti cha enzi cha Daudi kilikuwa.

Ufalme wa Daudi utakuwa wa milele

Ufalme wa Daudi ulikuwa ufalme wa Israeli na Yuda. Ulikuweko kwa miaka kadhaa. Baadaye watu walichukuliwa mateka kule Babeli. Yesu atakaporudi hapa duniani, atasimamisha Ufalme wa Mungu. Ufalme wa Mungu utakuwa wa milele.

Mungu atakuwa Baba wa wazao wa Daudi; na mzao wa kipekee atakuwa Mwana wa Mungu.

Mungu ndiye Baba wa Yesu Kristo. Yesu ndiye Mwana wa Mungu